# HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. SAMIA SULUHU HASSAN, RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KWA WAANDISHI WA HABARI BAADA YA ZIARA YA MHESHIMIWA KLAUS IOHANNIS, RAIS WA JAMHURI YA ROMANIA NCHINI TANZANIA

**TAREHE 17 NOVEMBA 2023**

***Ninatambua uwepo wa Mheshimiwa Klaus Iohannis, Rais wa Jamhuri ya Romania,***

***Waheshimiwa Mawaziri wa Romania na Tanzania,***

***Waheshimiwa Mabalozi wa Romania na Tanzania,***

***Wageni waalikwa,***

***Waandishi wa Habari,***

***Mabibi na Mabwana,***

**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!**

Kwa niaba ya Wananchi na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ninayo furaha kubwa kumkaribisha Mheshimiwa Klaus Iohannis, Rais wa Jamhuri ya Romania

pamoja na ujumbe wake hapa nchini. **Mheshimiwa Rais,** tunayo furaha kubwa kukupokea wewe na ujumbe wako hapa Tanzania, na hususan hapa Dar es Salaam.

***Ndugu Waandishi wa Habari,***

***Mabibi na mabwana,***

Uhusiano kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Romania, ulianza Mwezi Mei, 1964; yaani mwezi moja tu baada ya Muungano wa iliyokuwa Tanganyika na Zanzibar na kuundwa kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Romania imekuwa mbia wetu kama nchi, na pia kama Nchi Mwanachama wa Umoja wa Ulaya. Hivyo, ni dhamira yetu kuendelea kuimarisha uhusiano huo.

Ni kwa msingi huo, ziara hii ya Rais Klaus Iohannis ina umuhimu mkubwa sana kwa uhusiano wa nchi zetu mbili. Tumefurahi sana kumpokea, na ninakushukuru sana, Rais Klaus Iohannis kwa kututembelea. Kama mnavyojua, hii ni ziara ya kwanza ya Mkuu wa Nchi wa Romania kuja Tanzania. Kwa hiyo, ni ziara ya kihistoria.

Mazungumzo yetu ya leo, yalijikita kwenye masuala mbalimbali yenye umuhimu kwa nchi zetu mbili. Tumekubaliana kuendelea kuchukua hatua za pamoja ili kuimarisha zaidi uhusiano wetu kwenye maeneo ya kimkakati. Tumezungumzia fursa zilizopo kwenye sekta ya afya na utengenezaji wa madawa, usindikaji wa mazao ya kilimo, na fursa za kubadilishana uzoefu katika sekta ya kilimo, sekta ya madini, na pia katika kukabiliana na majanga kama mlivyoshuhudia mkataba umesainiwa hapa.

Tumezungumzia pia kuhusu kuongeza wigo wa ufadhili wa masomo hususan kwenye fani za udaktari na famasia. Kutokana na uhusiano mzuri Romania imekubali kutoa nafasi 10 za masomo kwa Watanzania katika maeneo ambayo tutayachagua. Kwa msingi wa rudisha hisani (*reciprocity*), nasi Tanzania tumetoa nafasi 5 kwa ajili ya vijana wa Romania kuja Tanzania kwenye maeneo na vyuo watakavyovichagua. Hatua hii itachangia jitihada zetu za kujengeana uwezo wa rasilimali watu na kuboresha huduma zetu katika sekta mbalimbali.

Ili kuimarisha zaidi uhusiano wetu, tumeshuhudia utiaji saini wa Hati mbili za Makubaliano kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Romania. Hati hizi zinahusu ushirikiano katika utafiti kwenye sekta ya kilimo, usalama wa chakula (food safety), na kukabiliana na majanga au dharura. Ushirikiano huu unalenga kuimarisha uwezo wetu kwenye sekta za kilimo na kukabiliana na maafa.

Tulizungumzia pia uhusiano wetu kwenye sekta ya biashara na uwekezaji. Kimsingi tumekuwa tukifanya kazi pamoja, lakini urari wa biashara umekuwa mdogo zaidi ukilinganisha na nafasi au fursa zilizopo. Tumezungumzia kukuza zaidi biashara, kuangalia maeneo amabyo tunaweza kufanya pamoja, kualika wafanyabiasahra wa Romania waje Tanzania au Watanzania waende Romania, ili wajadiliane na waone maeneo gani ambayo wanaweza kufanya kazi kwa pamoja.

Eneo lingine ambalo tumelizungumzia, ni majukwaa ya ushirikiano kimataifa. Tulizungumza na kujadiliana pia kuhusu namna tunavyoweza kuimarisha uhusiano wetu katika

majukwaa ya kimataifa. Nimepongeza azma ya Serikali ya Romania kuimarisha uhusiano na nchi za Afrika, ikiwa ni kiashiria kingine cha umuhimu wa Bara la Afrika katika ulingo wa kimataifa. Tumekubaliana kwamba, Mawaziri wetu wa Mambo ya Nje waendelee kukutana mara kwa mara ili kuzipa Serikali zetu mbili fursa za kufanya mashauriano kuhusu masuala ya kimataifa yenye umuhimu kwetu sote.

Tumezungumzia pia ushiriki wetu kwenye COP28 (Mkutano wa 28 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mabadiliko ya Tabianchi) ambayo utafanyika pale UAE (Umoja wa Falme za Kiarabu). Tumezungumzia maeneo gani ambayo tupeane nguvu kwenye mkutano ule. La muhimu zaidi, tumewaomba watusaidie kuzungumza na kutupa nguvu katika kuhakikisha kuwa lile tunaloenda nalo Tanzania, suala la **nishati** na **nishati safi ya kupikia**, lipate nguvu na tupate msaada kwa nguvu zote. Lengo ni kupunguza athari zinazojitokeza. Romania imesema kwamba wana majanga kama ya kwetu, kwa hiyo tushirikiane kuyasemea na kupata nguvu.

***Ndugu Waandishi wa Habari,***

Sisi na Romaia tulisaini Hati ya Makubaliano ya Mazungumzo ya Kisiasa baina ya nchi zetu mbili mwaka 2018. Katika mazungumzo yetu tumekubaliana sasa tuanze na Mkutano wa kwanza mazungumzo yale na tuone tunakwendaje mbele katika kukuza uhusiano na ushirikiano baina ya nchi zetu mbili.

Nikihitimisha, nimshukuru tena Rais Klaus Iohannis kwa kukubali mwaliko wangu na kwa kufanya ziara hii na kwa mazungumzo ya kina na mazuri baina ya pande mbili. Ni matumanii yangu kwamba yatokanayo na mazungumzo haya yatatoa msukumo mpya katika uhusiano wetu. Nami kwa upande wetu, nimhakikishie Mheshimiwa Rais Iohannis, kwamba Serikali ya Tanzaina tuko tayari kuimarisha uhusiano na Serikali ya Romania.

Katika ziara yake Rais Klaus Iohannis atatembelea pia upande wa pili wa Muungano, yaani Zanzibar. Akiwa kule Tanzania Zanzibar, pamoja na mambo mengine anatarajia kufanya mazungumzo na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la

Mapinduzi. Kwa upande wetu kama Tanzania, tumeisemea Zanzibar kwenye maeneo ya Uchumi wa Bluu na Utalii, kwa sababu ndio sekta zinazopandisha uchumi wa Zanzibar, na tumeainisha maeneo ambayo yangefaa kwa ushirikiano. Mengi zaidi, kwa sababu (Rais Iohannis) anakwenda Zanzibar, atayasikia kutoka kwa Rais (Dkt. Hussein Ali Mwinyi) mwenyewe.

Hivyo, ninamtakia safari njema na ziara njema anapotembelea Zanzibar.

Baada ya kusema hayo, sasa, ninayo heshima kukukaribisha Mheshimiwa Rais uzungumze na waandishi wa habari.

**Karibu sana Mheshimiwa Rais.**